

MANA ILISITISHWA NDANI NCHI YA AHADI

Kutoka 16:35

Wana wa Israil walikula mana muda wa miaka arobaini, hata walipofikia nchi iliyo na watu, wakala, ile mana hata walipofika mipakani mwa nchi ya Kanaani.

Sikia kile asemacho Nabii.

Yeye alikuwa akiwabariki Israel pengine hadi siku ile walipokataa kupanda juu kule kuitwaa ile nchi ya ahadi. Siku ile ile walipoacha kuwaamini wapelelezi, ile mana ilianguka vilevile usiku ule lakini walikuwa kwa ujumla nje ya mapenzi ya Bwana. Wasingeweza kushinda pigano jingine (vita vingine) hadi warudi na kuweka mambo yao kuwa sahihi na Mungu. Sasa, nafikiri ni wakati wa kanisa kurudi kwa Mungu tena. Iirudi na lianze kama lilivyokusudiwa kwenda, ili tuweze kuendelea na safari yetu [1]

Waza, lilivyo kamilifu, jinsi ambavyo wangeweza kuwa wakitembea kila siku, wakitembea na Bwana. Maisha ya jinsi gani ya kuishi, hapo ndani ya lile jangwa. Kula manna ya asubuhi, ambayo huanguka wakati wa usiku (kutoka 16).[2]

Hap ndipo walipofanya kosa lao, walipofika kwenye kiti cha hukumu na kuleta ule ushuhuda wa nchi njema (hesabu 13,14:1 – 12) ninafuraha kuwa kulikuwa na watu miaka iliyopita, ambao walikubali kupitia taratibu zote na walikwea na kumiliki ile nchi na kuchukua ushuhuda na kurudi, kwamba kuna nchi ng'ambo ya Mto Amen. Wanafurahia hilo. Sasa, walifanya kosa lao kubwa walipMManza kunung'unika dhidi ya

Musa na dhidi ya watumishi wa Mungu na dhidi ya Mungu, na likawaruka wao. Na kumbuka. Kila mmoja wao ambae alinung'unika hakuvingia kwenye Nchi ya Ahadi. Yesu alipokuwa hapa duniani, alisema "Baba zenu walikula manna jangwani. lakini kila mmoja amekufa lakini mimi ni Ule mkate wa uzima ambao unatoka kwa Mungu Mbinguni ambao mtu akiula hatakufa. (Yoh. 6:48 – 58) Oh nalipenda hilo. Kuvuka kutoka mautini kuingia uzimani, kuwa kiumbe kipya cha Yesu Kristo (Yoh 5: 24) [3]

Kumbuka, Israel walisafiri. Unakumbuka umbali waliokuja? Wangeweza kuwa Walikuwa maili arobaini tuu (40). Karibu miaka arobaini wakifanya hivyo (wakitembea) kwanini? Kwasababu walianza kunung'unika kinyume na sauti ambayo ilitoa ile ishara. Kidogo kiasi gani walichojua, wakati wakishangilia ukingoni mwa bahari na kucheza katika roho, na Musa akiimba katika roho ilikuwa ni siku chache tu zimepita. Lakini wakaanza kunung'unika, na wakataka kufanya kitu kingine tofauti. Na walikaa miaka arobaini Jangwani na kuangamia kwa ajili ya hilo walilo fanya (hiyo ni sawa) kwasababu hawakuamini Mungu alisema, hawaneni kinyume na wewe musa, wana nena kinyume na mimi "hiyo ilikuwa sauti ya Mungu na siyo ya musa (1Kor 10:1 -13) [4]

Wakati Israeli walipotoka Misri wote waliamini ujumbe wa nabii mmoja. Waliona ishara ya Mungu kwa Musa; kila mmoja na kila mmoja alitoka Misri, na wakavuka kwa miguu bahari ya shamu, walibatizwa wawe wa Musa, kila mmoja aliona nguvu za Mungu ikiwagusa wakati walipo imba katika roho na wakati Miriam alipo piga matari, akikimbia juu na chini katika pwani. Kila mmoja wao kila siku alikula mana mpya iliyotoka Mawinguni, kila mmojawao aliunywea ule mwamba wa kiroho ambao ulipigwa. Na kulikuwa na watu million mbili waliotoka Misri. Wangapi waliingia Nchi ya Ahadi wawili,mmoja

katika milioni. Wengine waliishia wapi? Yesu alisema waliangamia. “Baba zenu waliila mana jangwani kwa miaka arobaini, na nawaambieni ninyi, wote walikufa”

Sasa, kuna karibu wakristo million mia tano duniani leo tukihasabu wakatoliki na waprotestant na wote, kama Yesu angekuja kwenye unyakuo, kulingana na kile nimesema sasa hivi, wangukuwa watu miantano wametoweka ulimwenguni siku ya leo kwa kunyakuliwa. Na bila shaka ni hivyo kila siku. Ukihasabu nchi zote, ambazo hazikuwajibishwa kwa hiyo ingeweza kutokea wakati wowote, unaona?

Oh waKristo, hebu tuvae silaha za Mungu (Waef. 6:11 – 20) hebu tufanye yote tuwezayo kufanya kumtumikia Yeye, tumpende Yeye, na tusingoja ule wakati mkuu. Lakini Mungu atakufanikisha wewe, kwanini, Yeye amenibariki mimi” sinashaka na hilo Yeye alimbariki Balaam pia (Hesabu 22) unaona? Hakika Yeye yu radhi, utatembea katika mpenzi yake makamilifu, Mungu habadilishi nia yake, sababu Yeye amekubariki wewe. Yeye alimbariki Israeli moja kwa moja toka huko kwa miaka arobaini. Walifanya nini? Walioa wake, wakakuza familia, wakabusu watoto walilipa mafungu yao ya kumi, wakiishi vizuri kule na Mungu aliwabariki wao jangwani. Aliwalisha manna siku kwa siku, na kila mmoja wao aliangamia, sababu hawakutunza mapenzi yake makamilifu (yale ya kwanza) Neno lake la asili wakichukuwa mapenzi yake ya kuachilia [5]

Wamekuwa kama wana wa Israeli waliotoka Misri na wasifike nchi ya ahadi. Sasa wale wana wa Israeli waliotoka misri walikuwa karibu million mbili wenye nguvu. Wote walisafiri pamoja, wote waliona miujiza ile ile ya Mungu, wote walishiriki manna ileile na maji toka kwenye mwamba uliopigwa, wote walifuata wingu lile lile mchana, na nguzo ya moto usiku. (Kutoka 13: 21-22, 14:24) lakini wawili tu walifika ile nchi ya ahadi.

Wawili tu walikuwa waaminio halisi. hiyo ni sahihi kwa sababu Neno linakwambia wangineo waliangamia kwa sababu ya kutokuamini, na kwa sababu ya kutokuamini hawakuweza kuingia (waibrania 3:19) kama ili kuwa hivyo, ni wawili tu walioingia, hivyo waliosalia hawakuwa waaminio halisi. Kitu gani kilicho watofautisha? Wawili walikaa na Neno wakati mioyo ya wapelelezi kumi iliposhindwa hapo kadesh Banea, Joshua na kalebu hawakusitasila kwa kuwa waliamini Neno na kusema, tuna zaidi ya uwezo kuitwaa ile nchi” walijua wangeweza kwa sababu Mungu amesema, nimewapa ninyi nchi” (Kutoka 3: 7 – 8, 17) hata hivyo Waisraeli waliona nguvu na wema na ukombozi wa Mungu hawakuingia katika raha, ambayo ni mfano wa Roho Mtakatifu, sasa unaweza hivi sasa, kuwambia wachache sana wataamini moja kwa moja hata kupokea Roho wa Mungu. [6]

Mungu anawajibika kutunza ahadi yake. Wakati Mungu alipowatowa Israeli na kuwaleta jangwani, yeye aliahidi kuwa atawatunza. Na kile Mungu alichio ahidi ana kuwajibika kukitenda.

Wakati walipohitaji maji, walienda kwenye mwamba, walipo hitaji chakula, Mungu alinyesha Manna toka Mbinguni. Yeye alifungua bahari ya shamu. Angalia manna inayoshuka chini, ni mfano mzuri jinsi gani wa kanisa letu siku hii ya leo, kama Mungu alivyowaongoza Israeli kiasilia, anaongoza kanisa leo kiroho [7]

Sasa Paulo anaongea na wale Israeli wa kiroho ambao wamemiliki ile nchi. Oh hamna furaha kuwa mmetoka na kuacha vitunguu saumu vya misri? Hamfurahii mmetoka jangwani? Na kumbuka, iliwabidi waile Manna, chakula cha malaika toka mbinguni, mpaka walipovuka na kuingia nchini (Joshua 5: 10 – 13) na walipovuka na kuingia nchini, mana iliacha kuanguka. Walikuwa wamekomaa kikamilifu hapo, na walikula mazao ya kale ya nchi. Sasa, si watoto tena, kwamba mnatamani yale maziwa manyenyekevu ya ile injili, kwamba

hampaswi kuwa mnabembelezwa na kupigwapigwa na kuombwa kuja kanisani, sasa kwamba ninyi wa wakristo mliokomaa mko tayari kula nyama ngumu sasa (waibrania 5:12 – 14:6: 1-3) mko tayari kuingia katika kitu fulani. Yeye amesema. Mko tayari kuelewa mambo ya kina na ya utajiri. Oh tutaliingilia hilo moja kwa moja na, Oh, lilikuwa limefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alisema . "sasa tumekuja katika hili mimi nawaambieni ninyi, " sio wale ambao wametoka misri sasa, sio kwa wale ambao bado wamo safarini. Lakini wale ambao wamo ndani ya ahadi, wale walioipokea ile ahadi (1Kor 2:6 – 10)

Wangapi walioipokea ile ahadi ya Roho Mtakatifu? Na hamfurahi kuwa mko katika ile nchi mko hapa sasa, mnakula ZILI MBEGU ZA KALE, MKILA MAMBO YENYE NGUVU YA MUNGU, NA MNAELEWA WAZI WAZI. Akili zenu za kiroho zimefunikwa. Mnamjua hasa kuwa Yeye ni nani. Mnajua hasa mamlaka yake. Mnajua hasa wapi mnapoenda. Mnajua hasa yote kuhusu haya (Efes. 1: 15 – 23) [8]

Tazama: wandugu. KWA MUDA GANI HUU MANA ILIDUMU? Ilikuwapo katika safari yote, mpaka walipofikia majira mengine hadi kuingia nchi ya ahadi. Na hii itadumu muda gani? Mpaka Yesu atakapokuja. Petro alisema Tubuni kila mmoja wenu mkabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa sababu ahadi hii ni kwa ajili yenu na watoto wenu na kwa wale wote walio mbali na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie na kwa kadiri ya kizazi hiki kitavyodumu, Mungu bado anaita wanaume na wanawake kwenye kazi yake Yeye. [9]

Nukuu za kiingereza

[1] Kuthubutu" (62 – 0117) par E – 48

[2] Ninyi mnasema huyu ni nani? (64 – 1227), par 150 –

153

[3] Nena na ule mwamba (60 – 0723) par E – 25

[4] Sauti ya ishara (64 – 0321E) par E – 30

[5] Je, Mungu hubadilisha nia yake " (64 – 0321 E), par 12 – 14,177

[6] Wakati wa kanisa la Smirna CAB pg 148

[7] Kule kufufuliwa kwa Lazaro (51-0729 A) par E – 64

[8] Kufanywa wana (60 -0515 E) par 66 – 67)

[9] Maisha yaliyofichwa "(55 – 1006 A) par E – 35

Jiwe la kujengea la kiroho nambari 190 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendstr. 69.D-75328 Schomberge Germany Simu (+49) 2357613 Fax 72353306.

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk.)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa: Charles E. Y. Kanju

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@livel.com

Cellphone: 0784 704299/ 0713230098